

KRISTO ALIYETAMBULISHWA

KATIKA NYAKATI ZOTE



Maandiko machache hapa ambayo ninataka kuyarejea usiku wa leo. Nilikuwa nikiwazia juu ya somo la kwa nini tupo hapa. Ninataka kusoma sehemu ya Maandiko, ambayo ninaamini ya kwamba yote, katika kila mkutano, Neno la Mungu linapaswa kusomwa. Kwa sababu, ninajua Yeye angeweza kukutana nasi bila ya kusoma Neno, lakini ninahofu sana kwamba nitafanya kosa. Kwa hiyo kama nikilisoma Neno Lake, ninajua hakuna kosa katika Hilo. Kwa hiyo mimi—mimi hulisoma Neno Lake, ndipo ninajua ya kwamba jambo fulani litatoka kwenye mkutano huo, kwa sababu ya kusomwa kwa Neno Lake.

² Na kwa hiyo, tukiwekea msingi mawazo yetu juu ya Maandiko ambayo tutasoma, mahali pamoja panapatikana katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 10, kuanzia kifungu cha 32 na cha 39, vyote pamoja; halafu katika fungu la kale linalojulikana, Waebrania 13:8. Sasa katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 10, kuanzia kifungu cha 32, tunasoma haya.

Yesu akawajibu, Kazi njema nyingi nimewaonyesha, zitokazo kwa Baba Yangu; kwa ajili ya kazi ipi katika hizo mnanipiga kwa mawe?

Wayahudi wakamjibu, Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru, na kwa sababu...wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu.

Yesu akawajibu, Je! haikuandikwa katika torati yenu kwamba, Mimi nimesema, Ndinyi miungu?

Ikiwa aliwaita miungu wale waliojiliwa na Neno la Mungu, (na maandiko hayawezi kutanguka);

Je! Yeye ambaye Baba alimtakasa, akamtuma uliwenguni, ninyi mnamwambia, Unakufuru; kwa sababu nalisema, Mimi ni Mwana wa Mungu?

Kama sizitendi kazi za Baba yangu, msiniamini;

Lakini nikizitenda, ijapokuwa hamniamini mimi, ziaminini zile kazi; mpate kujua na kufahamu ya kuwa Baba yu ndani yangu, nami ni ndani ya Baba.

Wakatafuta tena kumkamata; lakini akatoka mikononi mwao.

³ Na katika Waebrania, mlango wa 13 na kifungu cha 8.

Yesu Kristo yeye yule jana . . . leo, na hata milele.

⁴ Hebu na tuombe. Baba wa Mbinguni, mtakase mjumbe usiku wa leo, Bwana, kwa Ujumbe, na mwenye kulisikia Neno, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁵ Sasa tunapolikaribia somo hili, somo dogo tu la kawaida kwa ajili ya usiku wa kwanza, tupate kufahamiana, ninataka kuchukua somo hili, la ninii . . . *Kristo Aliyetambulishwa Katika Nyakati Zote.*

⁶ Sasa Kitabu cha Waebrania hapa kinatwambia ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁷ Na tunasoma katika Biblia hapa ya kwamba Wayahudi hawa walikuwa wakimwuliza maswali. Tunaona Wayunani walimwuliza maswali. Na lilikuwa ni swali la sikuzote. Ilikuwa ni kwa sababu watu wengi sana wana fasiri nyingi sana za Yeye.

⁸ Hakuna mtu aliyepata kusikia habari Zake pasipo kutamani kumwona. Nina hakika ya kwamba kama ningaliuliza usiku wa leo, “Ni wangapi wenu wangetaka kumwona Yesu?” kila mkono ungeinuliwa. Hakuna ninii—hakuna mtu aliyepata kusikia habari Zake pasipo kutamani kumwona.

⁹ Kuna jambo fulani kuhusu hata Jina Lake, ambalo huninii tu . . . linatuvutia tu sana. Kuna kitu fulani kulihusu ambacho huusisimua moyo wetu, kulisikia tu Jina hilo, Yesu. Kwa sababu, katika Jina hilo tuna msamaha wa dhambi, tuna ukombozi wetu, kwa kuwa familia yote Mbinguni itaninii . . . inaitwa kwa Jina hilo. Na kwa hiyo sisi . . . Mungu kulichukua Jina hili la kibinadamu liwekwe juu Yake Mwenyewe wakati alipodhihirishwa katika mwili. Ni Jina la ajabu jinsi gani!

¹⁰ Sasa tuna—tunamwazia Yeye kuwa ni mkuu sana! Na kote katika nyakati, watu wote wamelilia kumwona Mungu. Sasa shida yake, tangu wakati wa Ayubu . . .

¹¹ Nafikiri Ayubu kinahesabiwa kuwa kimojawapo cha Vitabu vya kale kabisa katika Biblia. Kiliwekwa tu ndani. Kiliandikwa wakati wa Musa, Musa akiandika vile—vile vitabu vinne vya kwanza.

¹² Sasa tunaamini ya kwamba—ya kwamba Ayubu, mle ndani, alilia wakati mmoja, “Laiti ningaliweza tu kumwona! Laiti ningalijua mahali ningaliweza kwenda nyumbani Kwake! Ningetaka kwenda,” kwa maneno mengine, “nikabishe mlangoni Pake.”

¹³ Sote tunajua ya kwamba tunatoka mahali fulani. Tuko nyuma ya pazia fulani ambalo sisi . . . Kuna kitu fulani ndani yetu kinachotamani kushika kitu fulani, kwamba tunajua kwamba tunatoka mahali fulani. Hatuwezi kuwa kama tu tulivyo bila ya kuwepo na kitu nyuma yetu kutuumba.

¹⁴ Saa yangu isingaliweza tu kutukia. Mtu yeyote aliye na akili yake timamu angejua saa hiyo, vito, na mpangilio wa saa,

na virekebishaji, na springi, na—na mikono, isingalitukia tu. Haiwezekani kwake kutukia tu.

¹⁵ Angalia maumbile hayo mengine, jinsi yalivyopangiliwa vizuri pamoja. Tunajua hayangetukia tu kwa bahati. Ni zaidi sana jinsi gani mwanadamu alivyo mkuu kuliko saa! Mwanadamu ndiye aliyeibuni saa, na kuipimia wakati, na kuiunganisha. Kwa hiyo kama haiwezekani kwa saa hiyo kuwa ilitukia tu, ni zaidi sana vipi kwamba mimi na wewe ilitukia tu tukawa hapa? Hapana budi pawepo na muumba nyuma yetu. Kama tukiangalia uumbaji Wake mkuu, jinsi unavyosogea, na jinsi Yeye anavyoishi ndani yake, anavyoishi ndani yake.

¹⁶ Tunaona jani, jinsi ambavyo jani hujishikiza mtini. Na karibu na katikati ya Agosti, bila ya jalidi au chochote kile, uhai huliacha na kuingia chini mizizini. Jani hilo huanguka chini na kukaa papo hapo juu ya ardhi. Sasa kuna nini? Kuna akili fulani inayolizungumzia. Mti huo hauna akili yake wenyewe. Kwa hiyo uhai huingia chini kwenye mizizi ya mti, upate kujificha kutokana na hali ya hewa ya baridi. Kama huo... Kama ungalikaa huko juu, ungekufa, majira ya baridi kali yangualiuua.

¹⁷ Sasa jani hilo hufanya nini? Hulala ardhini na kuoza. Uhai hufanya nini wakati ukiwa kwenye mzizi? Huzinyonya kemikali hizo kutoka kwenye jani lililokufa, kalisi na chochote kile huingia ndani yake, kisha linachipuka tena katika majira ya kuchipua, na kurudi moja kwa moja mahali pake tena, ukichipusha jani lingine. Ni ushuhuda; mauti, kuzikwa na kufufuka.

¹⁸ Jua huchomoza asubuhi, kama mtoto mchanga aliyezaliwa. Saa mbili ama tatu liko shuleni. Saa nne limetoka shuleni. Saa sita liko kwenye umri wake wa makamu. Na kisha linaanza kufa, linakufa tena na kutua Magharibi. Je! huo ndio mwisho wake? Linafafuka kesho yake asubuhi, kushuhudia; uhai, mauti, mazishi, ufufuo. Kila kitu, yote, Mungu huishi katika maumbile Yake. Yeye hufanya hivyo na amefanya hivyo kote katika nyakati.

¹⁹ Sasa, njia moja pekee tutakavyopata kujua kama Mungu angali hai. Tunaweza kumwona katika uumbaji Wake, lakini Mungu alipataje kujionyesha kwa watu ya kwamba...

²⁰ Mtu fulani anasema, “Vema, Mungu yuko wapi? Unazungumza mengi sana kumhusu Yeye.”

²¹ Huko Afrika, kwenye huduma ya umishenari kule, na miongoni mwa Wa-Waafrikana, wanatumia neno la *amoya*, ambalo maana yake ni, “nguvu zisizoonekana,” kama vile upepo. “Mungu wako,” yeye anasema, “Mungu asiyeonekana, Yeye—Yeye ni kama upepo. Yeye ni nguvu, bali sisi—sisi hatumwoni.”

²² Vema, ninaamini ya kwamba tunaweza kumwona. Kwa sababu, tunaona katika mlango wa 12 wa Yohana Mtakatifu,

Wayunani fulani walikuja kumwona Yesu, nao wakasema, “Mabwana, tungependa kumwona Yesu,” ndipo wakapelekwa Kwake, na mmoja wa wanafunzi Wake. Na Waebrania 13:8 ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na kama anaweza kuchukuliwa katika siku hizo, akaonekane na mmoja wa wanafunzi Wake, kwa nini sisi tulio wanafunzi Wake, usiku wa leo, tusiwalete Mbele Zake wanaomtafuta, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Biblia inasema ndivyo alivyo, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²³ Sasa, ninajua hili linasikika la kijinga. Lakini kama mtatuvumilia tu kwa dakika chache, ninaamini ya kwamba mimi, kwa msaa wa Mungu, na Neno Lake na kulingana na Neno Lake, ninaweza kumleta papa hapa mbele zenu. Na halafu, jambo hilo, ni faraja ya jinsi gani! Hilo ndilo lililotuleta hapa. Sisi Wakristo tupo hapa kupata faraja, ku—kuleta, kuja katika Uwepo wa Mungu tunayemfahamu, ambaye anaweza kutufufua kama anavyolichipuza jani, anayeweza kuturejesha.

²⁴ Je! ni hadithi ya kutunga tu, ni baadhi tu ya maneno yaliyowekwa pamoja, ni hekaya fulani za Kiyahudi, ama ni Ukweli? Palipo na makosa mengi sana, hapana budi kuwepo na Ukweli mahali fulani. Palipo na dola bandia, nitasema kuna iliyo halisi ambayo hiyo imefanyizwa kuiigiza. Na palipo na kuigiza kwingi sana, na mambo mengi sana tunayoona siku hizi, hapana budi pawepo na Mungu aliye halisi mahali fulani.

²⁵ Sasa kama hatumtumikii, basi hebu na tuachane na jambo tunalofanya na twende tukamtumikie. Kwa sababu, hata hivyo, ushuhuda wetu unafaa nini kama haufai chochote? Na uaminifu wetu hauninii—hautuondoshi kwenye hukumu. Makafiri ni waaminifu. Watu hunywa asidi ya kaboliki wakati mwingine, ni waaminifu, wakifikiri wanakunywa kitu kingine. Uaminifu haufui dafu. Hapana budi pawe na njia iliyo sahihi, na njia iliyo mbaya.

²⁶ Ninaamini ya kwamba Biblia ni sahihi. Ninaamini ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Sasa Mungu hana budi kuhukumu. [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] Samahani. Hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kitu fulani.

²⁷ Sasa wakati nilipokuwa mvulana mdogo, familia yangu iliyonitangulia, sio baba na mama yangu, bali kabla ya hapo, tulikuwa Waairishi pande zote mbili, kwa hiyo, sisi, ilikuwa ni Katoliki na lilikuwa ni jambo la kawaida kwangu kulirudia kanisa Katoliki. Vema, baba na mama yangu walifunga ndoa nje ya kanisa, wala hawakwenda kanisani. Na basi nilipokuwa mtu mzima, kujua ya kwamba kulikuwako na Mungu, kama vile wengi wenu mlivyokwisha kusoma katika kitabu changu, ni—nilijua kulikuwako na Mungu mahali fulani.

²⁸ Lakini sasa, wazo la jambo hilo ni kwamba, kama Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa, basi litakuwa ni kanisa

lipi? Kama litakuwa ni kanisa Katoliki, basi ni kanisa la Katoliki ipi? Ya Kirumi, ya Kiorthodoksi, ama atauhukumu kwa ipi? Kama atauhukumu kwa la Kiprotestanti, je! ni ya Kimethodisti, Kibaptisti, Kipentekoste, Kipresbiteri? Ni ipi? Unaona, kuna kuchanganyikiwa kwingi mno.

²⁹ Kwa hiyo jamaa fulani angesema, “Vema, inaninii tu...” Loo, naam, injalisha. “Haijalishi, mradi tu wewe ni mwaminifu.”

³⁰ Kitabu cha kwanza kwenye Biblia, kilichosababisha mauti, magonjwa, huzuni, na dhambi, kilikuwa ni kwa sababu mtu mmoja hakuamini Neno moja. Katika Kitabu cha mwisho cha Biblia, Mungu yeye yule, katika Ufunuo 22, alisema, “Mtu atakayeondoa Neno moja, ama kuongeza neno moja Kwake, ataondolewa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Kwa hiyo hicho hakina budi kuwa ndicho Kitabu cha hukumu.

³¹ Sasa tunaona, ya kwamba, “Hapo mwanzo,” Yohana Mtakatifu 1, “hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Tulinwona, Mwana pekee atokaye kwa Baba, huyo Neno Mwenyewe, Mungu, alifanyika mwili na akakaa miongoni mwetu.”

³² Waebrania 13:8 inasema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Basi kama ni yeye yule, na ni Neno, basi Neno lilijitangazaje katika nyakati zingine zote? Itabidi Lenyewe lifanye vivyo hivyo leo, kuwa Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Hilo si zaidi ya Kweli. Yeye ni Neno; na ambapo, jinsi Neno lilivyotangazwa katika nyakati zingine zote. Mungu hajibadilishi. Malaki 1 ama... Malaki 3:6 inasema Yeye habadiliki. “Mimi ni Mungu, sina kigeugeu.”

³³ Kwa hiyo vile vile tu alivyokuwa hapo mwanzo, ndivyo alivyo leo. Naye alikuwa ni Neno, kwa jamii ya binadamu, hapo mwanzo. Mungu kamwe hakuipa jamii ya binadamu kanisa la kutegemea, kamwe hakuwapa kanuni za imani za kutegemea. Yeye alikuwa amemkinga mwanadamu kwa Neno Lake, “Aminini Neno hili mpate kuishi!” Ndilo jambo lile lile siku hizi. Basi Kristo Ndiye hilo Neno, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Sasa, kile Yeye alichokuwa katika nyakati zingine, basi hana budi kuwa yeye yule leo, kama anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele. Ambalo, nafikiri nimelielezea kinaganaga kabisa ya kwamba ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, na Yeye ni Neno.

³⁴ Sasa, Yesu alisema, “Maandiko hayangeweza kuvunjika.” Maandiko yalikuwa ni ya kweli. Nayo Maandiko yanasema, katika Yohana Mtakatifu 1, ya kwamba, “Neno alifanyika mwili, na akakaa miongoni mwetu.” Mungu alifanyika mwili, katika

Mwanawe, Yesu Kristo, na akakaa miongoni mwetu. Katika Yohana Mtakatifu 10:35, Yesu aliwaita wale aliowajilia, ambao walikuwa ni Neno hapo mwanzo, “manabii.” Yesu alisema hapa, “Torati yenu wenyewe inawafundisha ya kwamba, wale waliojiliwa na Neno la Mungu, nalo Neno la Mungu liliwajilia manabii.”

³⁵ Sasa Waebrania, mlango wa 1, inasema ya kwamba katika ninii... ilisema, “Mungu, katika nyakati mbalimbali,” na hizo ni nyakati za kale, “kwa njia mbalimbali alisema na baba zetu, kwa manabii; katika siku hizi za mwisho kwa Mwanawe, Yesu Kristo.” Unaona?

³⁶ Sasa, angalieni sasa, Mungu! Yesu alisema ya kwamba, “Wale waliojiliwa na Neno, waliitwa ‘miungu,’” hao walikuwa ni manabii. Sasa, si kwamba mtu huyo mwenyewe alikuwa ni Mungu, si zaidi ya vile mwili wa Yesu Kristo ulivyokuwa ni Mungu. Yeye alikuwa ni mwanadamu, Naye Mungu alikuwa amefunikwa nyuma yake.

³⁷ Mungu daima amejificha kutoka kwa watu wote, na kujifunua Mwenyewe kwa watu watakaoamini hilo. Mungu! Jumapili hii iliyopita, maskanini, nilihubiri juu ya *Mungu Aliyefunuliwa*. Mungu daima amejificha nyuma ya kitu fulani, kusudi watu wa ulimwengu wa nje wasijue lolote kumhusu Yeye. Bali anajifunua kwa watoto Wake na kwa wale walio radhi kuingia nyuma ya pazia hilo.

³⁸ Katika Agano la Kale kulikuwako na ngozi za pomboo ambazo zilimficha Mungu. Yeye alikuwa kwenye Utukufu wa Shekina. Huo ulikuwa nyuma ya ngozi za pomboo. Kabla hawajaingia nyuma ya ngozi za pomboo, walininii... .

³⁹ Neno lilikuwa ndani ya Musa, yule nabii. Yeye alipanda juu ya mlima. Alikuwa amekutana na ile Nguzo ya Moto, Nayo ikanena naye. Alishuka akaenda na kufanya ishara za nabii, akawaleta wana wa Israeli kutoka Misri, mpaka kwenye mlima huu. Na ndipo Mungu akashuka na kumtambulisha Musa, kwa kumwingiza katika hiyo Nguzo ya Moto, na akamficha Yeye. Hakuna mtu mwingine angaliweza kwenda. Hakuna mtu mwingine angalijaribu kuiga hilo, asingeweza kufanya hilo, walikufa. Mtu mmoja aliteuliwa, aliingia nyuma hapa, akaingia kwenye Nguzo ya Moto, akaingia katika Utukufu wa Mungu, na katika Utukufu wa Shekina; na alipotoka akiwa na hilo Neno kwa ajili ya wakati huo, alikuwa aking’ara sana kwa Utukufu wa Mungu hata ilimbidi kuufunika uso wake. Watu wasingeweza kumkazia macho. Na huo ulikuwa ni utaji wa maumbile ya kawaida.

⁴⁰ Ni kitu gani? Mtu anapovunja akapitia kwenye pazia hilo, akaingia katika Utukufu wa Shekina sasa, ulimwengu humwita mlokole. Hawawezi kuona kuna kasoro gani. Lakini huko nyuma, hakuna uzuri wa mtu huyo. Huenda asiyatamke maneno

yake ipasavyo. Hu—huenda asivalie ipasavyo. Huenda asivikwe mavazi ya kasisi. Mwanamke huenda asivalie jinsi wanavyoona anapaswa kuvalia. Huenda ikawa, lakini, mnaona, mle ndani, nyuma ya ngozi hiyo ya pomboo, nyuma ya ngozi hiyo ya kibinadamu, mle ndani mna ule Utukufu wa Shekina, mle ndani mna nguvu, mle ndani mna Neno, mle ndani mna mkate wa wonyesho. Na Utukufu wa Shekina, ambao ni Nuru, ambayo inaleta Nuru inayoivisha nafaka.

⁴¹ Ninyi watu wa Kansas mnajua jambo hilo, kwa mazao yenu ya ngano. Bila ya hilo jua, haitakomaa.

⁴² Na mpaka utakapokuja nyuma ya hiyo ngozi ya pomboo, mpaka utakapotoka nyuma ya ngozi yako ya kale, mawazo yako ya kale, kanuni zako za imani za kale, na uingie katika Uwepo wa Mungu; ndipo Neno linakuwa hali halisi iliyo hai kwako, ndipo umeinuka katika Utukufu wa Shekina, ndipo Biblia inakuwa ni Kitabu Kipya, ndipo Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaishi katika Uwepo Wake, ukila mkate wa wonyesho ambao unatolewa tu siku hiyo kwa waaminio, makuhani pekee. “Na sisi ni makuhani, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa kipekee, tukimtolea Mungu dhahihu za kiroho.” Lakini huna budi kuingia, huko nyuma ya pazia, upate kumwona Mungu aliyefunuliwa. Na Mungu anafunuliwa, hilo ni Neno Lake lililodhihirishwa.

⁴³ Sasa siku hizi tuna watu wengi sana wanaosema, “Vema, sisi, kama *akina nanii*, tunaliamini *hivi*.” Hilo kundi lingine linasema, “Sisi, kama *akina nanii*, tunaliamini *hivi*.” Unaona, unapata tafsiri nyingi sana!

⁴⁴ Mungu hahitaji mfasiri yeyote. Yeye hulifasiri Neno Lake Mwenyewe. Biblia inasema, “Si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote.” Mungu hufunua, Mwenyewe. Hufunua! Hapo mwanzo, Yeye alisema, “Iwe nuru,” na ikawa nuru. Hilo halihitaji fasiri yoyote. Mungu alisema, “Bikira atachukua mimba,” naye akachukua. Hilo halihitaji fasiri yoyote. Mungu alisema, “Katika siku za mwisho,” Yeye ange—“mwaga Roho” Wake “juu ya wote wenye mwili,” naye akammwaga. Hilo halihitaji fasiri yoyote.

⁴⁵ Lingali ni Neno! Neno ni Mungu. Mungu, katika kila wakati, amegawa kiasi fulani cha Neno Lake. Na mle ndani, angalia yale aliyofanya, Yeye alimtuma na—nabii. “Na Neno la Bwana humjia nabii.” Nabii hulifunua kwa wasikilizaji, nao wasikilizaji wanaliamini. Ndipo, basi, huyo ni Mungu katika matendo, Mungu akitenda kazi kwa Roho Wake.

⁴⁶ Sasa tunaona alijitambulisha Mwenyewe kama Mwana wa Adamu hapa, sasa, kutimiza. Sasa, wakati alipokuja duniani, kumbukeni, Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa umma, huko nje, alijitambulisha kama Mwana wa Adamu. Yeye alikuja katika majina matatu ya wana; alikuja kama Mwana wa

Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi. Sasa, *Mwana wa Adamu* ni “nabii.” Hata Yehova Mwenyewe alimwita Ezeieli, akasema, “Mwana wa Adamu.” Yehova, akisema na mwanadamu, nabii, alimwita, “Mwana wa Adamu.” Na Yesu alijitambulisha Mwenyewe kama Mwana wa Adamu, maana Maandiko hayawezi kutanguka.

Katika Kumbukumbu la Torati 18:15, Musa alisema, baada ya . . .

⁴⁷ Wana wa Israeli walisema, “Usimwache Mungu anene tena. Tunataka Musa anene nasi.”

⁴⁸ Yeye alisema, “Sitasema nao tena namna hiyo, bali nitawatumia Nabii.”

⁴⁹ Katika Kumbukumbu la Torati 18:15, yeye alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo Mimi.” Na kwa hiyo Andiko hilo haliwezi kutanguka, ilimbidi aje kama Mwana wa Adamu. Sasa hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wakati Wake, wakati alipokuwa hapa duniani.

⁵⁰ Ndipo wakati alipokufa, akafufuka, akapaa, kisha akamtuma Roho Mtakatifu, huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mungu ni Roho, na katika Wakati wa Kanisa imekuwa ni Mwana wa Mungu.

⁵¹ Halafu basi kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, ni Mwana wa Daudi, akiketi kwenye kiti cha enzi, akitawala. Yeye amepaa juu. “Yeye ashindaye ataketi pamoja Nami kwenye kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda, na ninaketi katika kiti cha enzi cha Baba Yangu.” Ameketi kwenye kiti cha enzi cha Baba sasa. Lakini katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Yeye ataketi kwenye Kiti Chake Mwenyewe cha enzi, kwa sababu Yeye ni Mwana wa Daudi.

⁵² Yeye ni Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi. Unaona, ni kamilifu kabisa.

⁵³ Sasa tunaona, ilibidi Yeye aje kama nabii. Kutokubadilika kwa Neno Lake! Mungu hana kigeugeu. Mungu habadiliki, kwa kuwa Yeye alikuwa Ndiye Nabii aliyekuwa ndani ya Yusufu. Alikuwa ni Nabii, alikuwa Mungu ndani ya Yusufu. Alikuwa Mungu ndani ya Daudi.

⁵⁴ Mwangalieni Yusufu, aliyaonyesha maisha ya Yesu karibu kikamilifu kabisa, bali alifanya kosa, ili kuonyesha ya kwamba haikuwa ni Yeye. Mwanadamu hufanya makosa. Mnaona, yeye alimwambia Farao, akasema . . . Alimwambia baba yake, ambaye alikuwa ni nabii, Yakobo, yeye alisema, “Mwambie Farao ya kwamba—ya kwamba sisi ni wachungaji wa wanyama, kwa sababu mchungaji ni chukizo kwa Mmisri.” Lakini huyo baba, Roho asingemruhusu kufanya hivyo; alisema, “Watumishi wako, wachungaji.” Kwa hiyo mnamwona Yusufu hapo akifanya kosa.

⁵⁵ Daudi, yule mtu mkuu, alifanya kosa. Mtu aupendezaye moyo wa Mungu, hata hivyo alimchukua Bathsheba, akifikiri angeweza kulificha jambo hilo kutoka kwa Mungu yeye yule aliyekuwa amemtumikia, maishani mwake mwote, bali Mungu alimfichua kwa nabii Nathani. Unaona?

⁵⁶ Lakini hata hivyo hebu mwangalieni Daudi wakati alipokuwa akitoka, amefukuzwa kutoka kwa watu wake mwenyewe, mfalme aliyekataliwa. Binti yake mwenyewe alikuwa amebakwa na kaka yake, na hao ndugu wengine wakamwua huyo kaka. Naye huyu hapa, Absalom alikuwa ameasi na kulitenganisha jeshi, akasababisha mapinduzi; na Daudi, baba yake mwenyewe, alikuwa amefukuzwa, akaondolewa, amekataliwa na watu wake. Alipokuwa akitoka mjini, maskini jamaa mmoja kiwete akijikokota pale, akimdhihaki, na kumtemea mate. Yule mlinzi aliuchomoa upanga wake, akasema, “Nitakiacha kichwa cha yule mbwa kikae juu yake, akimtemea mate mfalme wangu?”

Daudi akasema, “Mwache. Mungu alimwambia afanye hivyo.”

⁵⁷ Hapana shaka, Daudi hakujua alilokuwa akifanya; akatembea akikwea Mlima ule ule wa Mizeituni pale, kisha akaangalia chini, akilia, mfalme aliyekataliwa. Ambapo, miaka mia chache baada ya hapo, Yesu Kristo aliketi juu ya mlima ule ule, Mwana wa Daudi, akilia kama mfalme aliyekataliwa, nao wakamtemea mate, pia.

⁵⁸ Mnaona, mambo haya yote yalimwonyesha tu Kristo. Yeye alikuwa ni sehemu yake. Mungu habadiliki. Tabia Yake haibadiliki. Yeye angali ni Neno, mnaona, na Malaki 3:6 inathibitisha hilo. Yeye hubadilisha tu umbo lake kwa kila wakati. Kila wakati, Yeye ameweka sehemu ya Neno ambalo limetabiriwa litatukia katika siku fulani. Vema, wakati huo unapokuja, Mungu huingia tu katika umbo jingine. Unaona, ni Mungu wakati wote, lile Neno, “Neno lilifanyika mwili na likakaa kwetu.”

⁵⁹ Sasa katika Waebrania 4, tunaona, Waebrania 4:12. Yesu alitambulishwa kikamilifu kwa kazi Zake na yale aliyofanya, kwa kuwa Waebrania 4:12 inasema, kwamba, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili. Pia huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.”

⁶⁰ Hivyo ndivyo Ibrahimu, wakati mtu huyu alipokutana naye, akiwa na nguo Zake zimejaa mavumbi, na tunaona, wakati Ibrahimu alipomwona huyu Mtu, yeye alimwita kando.

⁶¹ Wawili wa hao walishuka kwenda Sodoma; picha nzuri sana ya siku hizi tunazoishi, na tunamwona Billy Graham mamboleo na hao wengine huko Sodoma, wakiwatoa.

⁶² Angalia kanisa lililoteuliwa, hata hivyo, ule uzao halisi wa Ibrahimu. Lutu alikuwa mpwa wake, lakini Ibrahimu...

Mtu Huyu kamwe hakushuka kwenda kule, Yule aliyezungumza na Ibrahimu. Na wakati alipozungumza na Ibrahimu, alisema, “Ibrahimu.” Sasa kumbukeni, jina lake lilikuwa ni *Abramu*, siku chache kabla ya hapo, na mkewe alikuwa ni *Sarai*, sio Sara.

Na Yeye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yumo hemani, nyuma Yako.”

⁶³ Akasema, “Nitakuzuru majira kama haya mwakani.”

Na Sara, moyoni mwake, kwa namna fulani akalicheka.

⁶⁴ “Ndipo Mtu huyo, akiwa ameelekeza mgongo wake kwenye hema,” Biblia ilisema, “akasema ‘Mbona Sara amecheka?’ hemani nyuma Yake.”

⁶⁵ Na Ibrahimu alimwita Mtu huyo “Elohimu.” *Elohimu* ni “Aishiye peke yake.”

⁶⁶ Sasa neno la Kiingereza *mungu* linamaanisha chochote. Hayo maneno ya Kiingereza, huna budi kuyaangalia, maana yana kila namna ya mawazo yaliyopotoshwa. Mungu, dawati hili lingeweza kuwa ni mungu, mti ungeweza kuwa ni mungu, mwanadamu angeweza kuwa ni mungu, chochote mungu, neno la Kiingereza mungu linamaanisha.

⁶⁷ Lakini *Elohimu* linamaanisha “anayeishi peke yake.” Kunaweza tu kuwako... Dawati hili haliishi peke yake. Mtu haishi peke yake. Mti hauishi peke yake. Bali Elohimu anaishi peke yake! Anayeishi peke Yake, aliyedhihirishwa katika mwili, amesimama pale, akila, akinywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, akila nyama, ndama, akila mkate, na akizungumza na Ibrahimu. Na Ibrahimu alisema alikuwa ni “Elohimu.”

⁶⁸ Naye Yesu, katika Luka Mtakatifu 17, alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kule kurudi, wakati Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa.” Si Mwana wa Mungu, sasa; “Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa”! “Wakati anapofunuliwa, anapotambulishwa kwa Kanisa Lake, Mwana wa Adamu atafunuliwa kabla tu ya Mwana aliyeahidiwa.”

⁶⁹ Ibrahimu alikuwa amemwona Mungu katika namna nyingi mbalimbali, katika Nuru, na katika maono; bali huyu hapa Mungu katika Mwanadamu, kabla tu ya yule mwana aliyengojewa na kuahidiwa kutokea.

⁷⁰ Yesu alisema, “Kabla ya kurudi tena kwa Mwana aliyeahidiwa, Elohimu angejifanya Mwenyewe (Neno Lake) kudhihirika katika mwili, Mungu!”

“Mabwana, tungetaka kumwona Yesu!”

⁷¹ Mungu akidhihirishwa vile vile katika nyakati zote, daima imekuwa, Yeye amejificha nyuma ya mwili wa mwanadamu. Ni Mungu ndani yako. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo mtaniona. Nitakuwa pamoja nanyi.”

Yeye hata yumo ndani yetu; atakuwa, hata ukamilifu wa dahari, mpaka atakapofunuliwa katika lile umbo akishuka kutoka Mbinguni.

⁷² Neno la Mungu la wakati huu, Yeye aliuahidi nini wakati huu? Kama ukiangalia katika Biblia na uone kile kilichoahidiwa kwa ajili ya wakati huu, na uone Hilo likiishi, sijali ni nani anayesema ni kweli ama ni makosa, Hilo ni kweli kwa sababu ni Mungu akilifasiri Neno Lake Mwenyewe.

⁷³ Hahitaji mtu yeyote kusema, “Vema, hizo siku zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Na huo wote ni ushupavu wa dini.” Ni—ni makosa! Mungu anaposema ya kwamba atafanya jambo hilo katika wakati fulani, Yeye atalifanya. Lakini jambo ni kwamba, tunaingia kwenye mkondo wa siku za kale wa kitu fulani huko nyuma, shule fulani kuu kutoka huko nyuma, nasi tunalikosa.

⁷⁴ Hiyo ndiyo sababu walimkosa Yesu wakati alipokuja. Wangali walikuwa wakijaribu kuishi chini ya Torati, wakati Biblia ilikuwa imeshasema wazi. . . Papa hapa, nitaisoma, Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo Ndiyo yanayonishuhudia. Maandiko yasiponishuhudia, basi ni uongo.” Hakika wengeweza kuona ya kwamba bikira atachukua mimba! Hakika Yeye alikuwa Ndiye jibu kamilifu kwa hayo Maandiko! Sisi Wakristo tunaamini jambo hilo sasa.

⁷⁵ Lakini ingalimfaa nini Musa kuja na siku ya Nuhu, Ujumbe wa Nuhu? Ingelimfaidi nini Yohana Mbatizaji kuja na ujumbe wa Musa? Unaona?

⁷⁶ Sisi hatuko kwenye ujumbe wa Sankey. Hatuko kwenye ujumbe wa Moody. Tuna Ujumbe wa saa hii! Hatuko kwenye ujumbe wa Luther au ujumbe wa Wesley. Walikuwa sawa, bali hii ni siku nyingine. Hii ni ahadi nyingine. Huu ni wakati mwingine wa kanisa. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele!” Jinsi lilivyo la ajabu sana, jinsi watu wanavyoweza kuwa vipofu, katika wakati huo, lakini haina budi kuwa hivyo. “Vuguvugu,” katika wakati huu, Biblia ilisema, “nao wangetapikwa kutoka kinywani Mwake,” katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia. “Bali wengi kadiri awapendao, Yeye huwarudi na kuwakemea.” Alisema kwamba ingekuwa jinsi hii katika wakati huu wa Kanisa la Laodikia.

⁷⁷ Kumbukeni, Mungu hubadilisha umbo Lake. *En morphé*, neno hilo la Kiyunani linamaanisha Yeye huvaa kinyago kingine. Kama vile katika *Carmen* ama kitu fulani, ama—ama tamthilia za Shakespeare, Yeye ni—Yeye ni kama mwigizaji, Yeye hubadilisha sura Yake. Yote yale hao manabii waliyokuwa, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya hao manabii. Yesu alisema hivyo, “Mnawaita ‘miungu,’ hao waliojiliwa na Neno la Mungu: Nami huyu hapa, Mwana wa Mungu, mnanihukumuje?” Loo, jamani!

⁷⁸ Ni jambo lile lile leo, ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, Ujumbe wa saa hii, Nuru ya siku hizi! Hatuwezi kuchukua hizo jumbe zingine za huko nyuma, tayari zimekwisha kuishiwa; tunaishi katika mng'ao wa nuru fulani.

⁷⁹ Hilo ndilo deni lililo kuu kabisa, unyang'anyi ulio mkuu kabisa, mataifa yaliopata kujua, ulifanyika Uingereza hapa si muda mrefu uliopita, ulifanywa kwa taa za bandia. Dola milioni saba, unyang'anyi wa garimoshi, haujapata kutukia hapo kabla, katika historia. Huo ulikuwa ni wizi mkubwa, dalili ya chanzo cha wakati wa wahalifu ulimwenguni.

⁸⁰ Na dalili iliyo kuu zaidi ya wahalifu katika wakati huu, katika ulimwengu tunamoishi, ni nuru bandia katika majira haya tunayoishi, inayotaribu kuturudisha nyuma chini ya namna fulani ya kanuni za imani na kadhalika. Wakati, sisi ni nyaraka zilizo hai, ama, kwa maneno mengine, sisi ni nyaraka ambazo ni hai, ambazo zimeandikwa na sasa zinaliishi Neno la Mungu, kama alivyoahidi katika majira haya; Neno lililodhihirishwa, nyaraka zilizoandikwa, ambazo zimekuwa zikiishi. Hicho ndicho wale mitume walichokuwa.

⁸¹ Hicho ndicho Yohana Mbatizaji alichokuwa. "Alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani." Alijaribu kuwaambia hilo. Yeye alikuwa pia ni Malaki 3, "Tazama, ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso wangu, akaitayarisha njia mbele ya watu." Yeye alikuwa ni lile Neno lililo hai.

⁸² Nalo kanisa la kweli lililozaliwa mara ya pili katika majira haya ndilo Neno la Mungu lililo hai. Ni Neno la wakati huu, lililodhihirishwa. Yachunguzeni Maandiko na mwone ni kitu gani kinachopaswa kuwapo katika wakati huu. Huyu hapo Kristo akiishi tena, akibadilisha tu kinyago Chake kutoka kimoja hadi kingine.

⁸³ Sasa, Yeye alitambulishwa kabisa kama Masihi. Walipaswa kujua hilo. Tunajua kile Masihi alichopaswa kuwa. Alipaswa kuwa ni Nabii. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema alikuwa. Hivyo ndivyo alivyosema alikuwa. "Mimi Mwana wa Adamu, mnasema Mimi Mwana wa Adamu kwamba ni nani?" Sikuzote anajitambulisha kama wakati wa Nabii, anajitambulisha kama Nabii wa Mungu. Hivyo ndivyo alivyokuwa.

⁸⁴ Lakini Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa ni Mungu-Nabii. Kile alichokuwa Daudi, kile alichokuwa Musa, kile alichokuwa Eliya, kile walichokuwa hao wote, "katika Yeye ulikaa utimilifu wa Ungu kwa jinsi ya mwili." Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii. Alikuwa ni Mungu, Yehova, aliyefanyika mwili katika Mwana Wake Mwenyewe, akajijengea maskani apate kujidhihirisha ndani yake. Wengine wote walishindwa, walikuwa na mapungufu; bali hakuna dosari ndani Yake. Hata Mungu Mwenyewe alisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ninayependezewa kuishi ndani Yake." Hiyo ni kweli,

hakuna dosari ndani Yake. “Msikieni Yeye!” Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa.

⁸⁵ Wao walisema, “Unajifanya Mwenyewe u Mungu, ama sawa na Mungu.” Alikuwa hivyo. Yeye alikuwa ni Mwanawe Mwenyewe. Amina. Alikuwa...Alikuwa ni dhihirisho la Mungu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

⁸⁶ Na katika siku hii ya mwisho, Yeye ananena na watu kupitia Mwanawe, Kristo Yesu, akijitambulisha Mwenyewe. Basi Kristo ni nini? Neno. Neno la nini, neno la Musa? Naam, bali siku hii Yeye ni Neno lililodhihirishwa kwa ajili ya siku hii.

⁸⁷ Angalia jinsi Yesu alivyokuwa. Sasa, Yeye anapaswa awe ni Nabii, hebu na tuone kama alikuwa na ishara ya Masihi. Hebu na twende katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 1, kwa dakika zingine tano, kumi, kabla hatujafunga. Yohana Mtakatifu 1, tunamwona Yeye akiya duniani. Alizaliwa na bikira, kile tu Biblia ilichosema. Alichukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la bikira.

⁸⁸ Si kwamba huyo bikira alikuwa ni mungu mke sasa, yeye. Unasema, “Na Mariamu je?” Hakuwa mkamilifu. Alikuwa ni mwanamke, mwanamke tu kama mwanamke mwingine yeyote, si mungu mke; mwanamke. Mtu fulani alisema, “Hivi huoni aibu kusema jambo hilo?” La, bwana!

⁸⁹ Angalieni hapa. Ni wapi alipokosea? Mbona, hili hapa moja alilofanya. Wakati waliposhuka kwenda kwenye sikukuu ya Pentekoste, nao hao watu wakaenda mwendo wa siku tatu; nao wakamkosa, wazazi Wake, ndipo wakarudi kwenda kumtafuta. Nao wakampata katika Maandiko, akihojiana juu ya Hayo na makuhani hekaluni. Basi angalieni yale Mariamu aliyosema, pale pale mbele ya wale makuhani, wale wakosoaji. Alisema, “Mimi na baba Yako tumekutafuta, kwa machozi.”

⁹⁰ Lakini Neno daima hulinyosha kosa. Yeye alikuwa ni Neno, Mvulana mwenye umri wa miaka kumi na miwili. Hekima hii ilitoka wapi?

⁹¹ Kumbukeni, papo hapo aliukanusha ushuhuda wake. Alisema Mungu Ndiye aliyekuwa Baba Yake; na hapa akasema, “Mimi na baba Yako, Yusufu, tumekutafuta, kwa machozi.”

⁹² Akasema, “Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwa kazini kwa Baba Yangu?” Unaona? Unaona? Kama angelikuwa na baba Yake, Yusufu, Yusufu angelikuwa ndiye baba Yake, angekuwa akitengeneza milango ya makabati na kadhalika. Unaona? Bali alikuwa katika shughuli za Baba Yake, akilinyoosha Neno la siku ile. Yeye alikuwa ni Neno. Amina. Unaona, Mariamu alikosea, bali hakuna makosa aliyofanya Yeye. Alikuwa ni Yule mkamilifu.

⁹³ Angalieni, hapo alipozaliwa, akalelewa, akabatizwa na Yohana, Roho Mtakatifu alimshukia, akaenda nyikani, akatoka, huduma Yake ikaanza, kuponya. Palikuwapo na mtu Jina lake Simoni, naye akaja pamoja na ndugu yake, Andrea, kwenye mkutano.

⁹⁴ Sasa sikilizeni kwa makini sasa, tunaenda kufunga—kufunga, na tuone kile alichokuwa wakati huo. Na kama “Alinena na baba zetu kwa manabii, katika siku hizi za mwisho kwa Mwanawe,” tuone tu kile Mungu alichokuwa siku hizi, tuone kama Yeye ametambulishwa jinsi ile ile.

⁹⁵ Yeye alijitambulishaje? Je! alishuka na kusema, “Sasa nimemaliza shule. Nimepata Digrii yangu ya kwanza ya Sanaa, Ph.D., LL., kadhalika. Niko tayari kwa huduma Yangu”? La, bwana. Hakufanya hivyo. Alikwenda nyikani, kama alivyofanya Yohana, akatoka ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu.

⁹⁶ Angalieni jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe wakati alipoanza kuhubiri. Kulikuwako na mtu mmoja, Andrea, aliyekuwa akimsikiliza Yohana, akashuka akaenda pamoja na Yesu kumtafuta alikokuwa, akamfuata mpaka kwenye mkutano; akamleta ndugu yake, Simoni. Mara Simoni alipofika Mbele za Yesu, Yesu akasema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni Mwana wa Yona.” Hilo lilimtambulisha. Papo hapo jina la Petro likabadilishwa kutoka Simoni likawa Petro, ambalo ni “jiwe dogo,” kisha akawa kiongozi wa kanisa, baadaye.

⁹⁷ Halafu tunamwona jamaa amesimama pale, jina lake Filipo, akasema, “Sasa ngoja kidogo, hatujakuwa na nabii kwa miaka mia nne. Nabii ajaye, tunajua jinsi atakavyokuwa.”

⁹⁸ Kwa hiyo basi anaenda nyuma ya milima, kama maili kumi na tano, kama ukipata kuwa pale kupaangalia mahali hapo, ambapo alimpata rafiki mmoja ambaye walikuwa na masomo ya Biblia pamoja naye. Alikuwa ni mtu mwaminifu sana, mzuri, aliyestaarabika. Jina lake lilikuwa ni Nathanaeli. Kwa hiyo hapana shaka, alienda mlangoni akakuta kwamba hakuwa nyumbani kwake, huenda ilikuwa ni mkewe aliyesema, “Yuko huko nje kwenye shamba lake la mizeituni, huko nje akiomba.”

⁹⁹ Kwa hiyo Filipo, huku amechochewa sana na yale aliyokuwa ameona yakifanywa, ule utambulisho mkamilifu wa Kumbukumbu la Torati 18:15, Nabii alikuwa ameinuka! Kwa hiyo akaenda, akakutana na Nathanaeli, na kusema, “Nathanaeli, njoo, uone Yeye tuliyempata.” Hawakuwa na wakati wa kuzungumza juu ya hali ya hewa na kadhalika. Ujumbe ulikuwa ni wa haraka. Moyo wake ulikuwa ukiwaka moto. Hilo ni jambo kuu sana sasa kwetu, tuna mambo mengi sana ya kufanya mbali na *Hili*. Na muda si muda mwajua, yeye alisema, “Njoo, umwone Yeye tuliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufo.”

¹⁰⁰ Hebu na tuyadukue mazungumzo yao wakati walipotembea ufukoni mwa bahari. Ninaweza kumsikia Filipo akimwambia Nathanaeli, “Je! unamjua yule mzee mvuvi kule chini, unajua?”

¹⁰¹ “Loo, yu—yu—yule mzee aliyekufa hapa si muda mrefu uliopita, Yona?”

“La, la. Mwanawe, Simoni.”

¹⁰² “Naam, Naam. Loo, ninakumbuka nikinunua samaki kutoka kwake. Vema, vipi kumhusu? Vema, hana elimu ya kutosha kuliandika jina lake mwenyewe. Asingeweza kutia sahihi risiti yangu.” (Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa, bali walijua ya kwamba alikuwa pamoja na Yesu; kwa hiyo tunaona hata asingaliweza kutia sahihi kwenye risiti.)

¹⁰³ Akasema, “Naam,” akasema, “unajua nini? Wakati alipokuja moja kwa moja mbele ya Mtu huyu, Mtu huyu bila kumfahamu, akamwambia jina lake lilikuwa ni ‘Simoni, mwana wa Yona.’” Kasema, “Haimkini Huyo Ndiye Masihi? Huyo si ni nabii? Hiyo si ni Kumbukumbu la Torati 18, kutimizwa kwa Maandiko? Hebu yafuatilie maisha Yake huko nyuma; tunaishi katika siku gani? Tunaishi, tukimtazamia yule Masihi ajaye. Sisi sote Waebrania tunakutazamia. Huyo si ndiye?”

¹⁰⁴ “A-ha, sasa ngoja kidogo,” Nathanaeli akasema, “Itanibidi kuchunguza.”

“Vema, halitanishangaza kama hatakuja.”

¹⁰⁵ “Ha-ha-ha, hebu nilione. Hebu nihudhurie mmoja wa mikutano nione hilo likitendwa.”

¹⁰⁶ Vema, anaenda moja kwa moja mkutanoni ambapo Yesu anasimama. Akasema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!”

Akasema, “Rabi, ulinijua lini?”

¹⁰⁷ Kasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.” Hilo lilitosha. Hilo lilitosha.

¹⁰⁸ Hilo ni nini? “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Mnaona, Yeye alijitambulisha Mwenyewe, lile Neno.

¹⁰⁹ Msomi huyu alisema nini? “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.”

¹¹⁰ Lakini hapo karibu walisimama baadhi ya wale, ambao hawakuamini hilo. Wakasema, “Mtu Huyu ni Beelzebuli.”

¹¹¹ Yesu akasema, “Ninawasamehe hilo, kumwita Roho wa Mungu ‘kitu kichafu,’” kwa kuwa upatanisho haukuwa umefanywa. “Lakini wakati Roho Mtakatifu, Yeye Roho Mtakatifu...” Yeye ni kiwakilishi nafsi; wakati, sio wazo; Mtu! “Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.” Kumbukeni, ni yeye yule jana, leo, na hata milele; Neno lililotambulishwa

likifanyika mwili. Ndipo tunamwona pale, sasa, hao walikuwa ni Wayahudi.

¹¹² Kuna jamii tatu tu za watu. Tunaweza kuwa na ubaguzi wetu na—na miungano, na lolote mtakalo, mimi... haliniyutii. Mimi ni mtumishi wa Kristo, nikiwatumikia watu wote. Lakini, sikilizeni, hebu niwaambie. Angalieni hapa. Kulikuwako na Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

¹¹³ Na hebu iangalieni Injili, ikizungumza juu ya Petro akiwa na zile funguo. Aliufungua kwenye Siku ya Pentekoste, kwa Wayahudi. Filipo akashuka na akaenda na kuwabatiza Wasamaria, na kutoa pepo, Roho Mtakatifu alikuwa hajawashukia; Petro akashuka akaenda na kuwawekea mikono, wakampokea Roho Mtakatifu. Na katika nyumba ya Kornelio, Wamataifa walimpokea.

¹¹⁴ Sasa, Wamataifa, sisi Wamataifa, sisi Waanglo-Sakson, hata hatukuwa tukimtarajia Masihi yeyote; tulikuwa makafiri, tukibeba marungu mgongoni mwetu, tulikuwa tukiabudu sanamu. Lakini wote wawili Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi.

¹¹⁵ Naye huwajia tu wale wanaomtazamia. Kumbukeni hilo kote katika mkutano huu, Yeye atakutana tu na wale wanaomtazamia!

¹¹⁶ Hatimaye, basi Yeye anahitaji... alikuwa akienda Yeriko siku moja, Naye alitaka kupitia Samaria, ambao uko huko nyuma ya milima. Akafika mahali pale... Sasa, tumemwona akijitambulisha Mwenyewe kama Masihi, akionyesha ishara Yake ya Masihi, nao wakaikufuru, kwa hiyo alitaka kupitia Samaria. Wao walikuwa wakimtazamia Masihi, pia. Kwa hiyo akaja kwenye mji ulioitwa Sikari, mnamo kama kwenye saa sita.

¹¹⁷ Kile kisima, kingali kiko pale, wanaketi tu chini karibu nacho, nje tu ya lango la jiji hilo. Ambapo, pampu ya umma, wote wanakuja kuchota maji yao; sio pampu, wao hushusha tu winchi na kuchota maji. Nao wana hayo mabalasi makubwa, wangali wanayo siku hizi. Na hebu nena kuhusu kutengemaa, baadhi yenu wanawake mnaotembea mmebeba vitabu kichwani mwenu? Mnapaswa kuona jinsi hao wanawake wanavyoweza kuweka balasi la galoni tano kichwani mwao, na moja kwenye kila nyonga, na kutembea tu, wakizungumza, na kuvitegemeza kikamilifu.

¹¹⁸ Nao wakishuka wakienda, mnamo saa tano mchana, ambapo walifika kule karibu saa sita, Naye akawatuma wanafunzi mjini wakanunue vyakula.

¹¹⁹ Basi kulikuwako na mwanamke fulani mjini, mwenye sifa mbaya, hakuruhusiwa kuwa pamoja na wanawake wengine, kwa hiyo akaja kisimani kujitekea maji. Na alipokuwa karibu kushusha mtungi wake wa maji, aliangalia, ameketi

pale akiegemea ukuta, Mwanamume aliyemsemesha, kasema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹²⁰ Sasa, walikuwa na ubaguzi mkali, Wayahudi na—na Wasamaria. Naye akamjulisha, upesi sana, ya kwamba—ya kwamba haikuwa desturi kwa Mwanamume wa sampuli Yake kumwomba mwanamke kama yeye, Msamaria, kibali chochote, kwa sababu Wayahudi na Wasamaria hawakupendana, hawakuwa na ushirikiano wowote. Akasema, “Lakini kama ulijua ni nani unayesema Naye, ungeniomba Mimi maji unywe, Nami ningekupa maji usiyokuja hapa kuchota.”

¹²¹ Yeye alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho ya huyo mwanamke. Yeye alikuwa ni nabii. Nao mjadala ulikuwa kama wanapaswa kuabudia Yerusalemu ama mlimani. Akasema, “Baba anawatafuta hao watakaoabudu katika Roho na Kweli.”

¹²² Ndipo akaendelea mpaka akapata shida ya mwanamke huyo ilikuwa ni nini. Aliendelea moja kwa moja mpaka akapata shida yake. Sote tunajua ilikuwa ni kitu gani, sisi tunaoisoma Biblia, Yohana Mtakatifu 4. Tulipata nini? Alikuwa na waume wengi mno. Akasema, “Nenda kamwite mume wako mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

Akasema, “Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano.”

¹²³ Angalieni tofauti kati ya mwanamke huyo na hao makuhani katika siku ile. Alisema, “Bwana, naona ya kuwa U nabii. Sasa hatujakuwa na mmoja kwa miaka mia nne. Naona ya kuwa U nabii. Tunajua Masihi ajapo, hili ndilo jambo atakalofanya.” Hiyo ni kweli? “Yeye atatuonyesha mambo haya. Atatwambia jambo hili.”

Akasema, “Mimi Ndiye, ninayesema nawe.”

¹²⁴ Mtu tu wa kawaida ameketi pale, mwenye umri wa miaka thelathini tu; labda alionekana ni wa hamsini, maana walikuwa ndiyo kwanza waseme, katika Yohana Mtakatifu 6, “Wewe ni Mtu usiyepata bado miaka hamsini, Nawe unasema umemwona Ibrahimu, sasa tunajua ya kwamba Wewe una pepo.”

Lakini akasema, “Ibrahimu asijakuwapo, MIMI NIKO.”

¹²⁵ Na, naam, huyo hapo, ni jamaa mdogo tu, labda akiingia mvi kidogo ndevuni Mwake, kazi Yake; mwili Wake wa kibinadamu ulikuwa ni mnyonge, “Hana uzuri hata tumtamani,” ngozi ya kale ya pomboo tena; bali kilichokuwa ndani yake kilikuwa ni Shekina, kilichokuwa ndani yake kilikuwa ni Mungu. Mungu! Ilikuwa ni kitu gani? Huyo hapo ametambulishwa, Neno la Mungu, akijua siri za moyo wao. Mnaona, hilo lilikuwa ni Neno la Mungu. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu.

¹²⁶ Na Neno la Mungu lingali linafanya jambo hilo, kwa sababu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mnaliona, mnaliona

katika mawazo yenu sasa? Angalieni, “yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹²⁷ Alikimbilia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia yale nimefanya. Haimkini huyu kuwa Ndiye Masihi?”

¹²⁸ Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi, kwa Myahudi na kwa...na kwa M—Msamaria; na Yeye hana upendeleo, ni yeye yule jana, leo, na hata milele; na huo ulikuwa ndio mwisho, wakati Mungu alipoacha kujishughulisha na Wayahudi na Wasamaria. Na huo ndio mwisho wa kipindi cha wakati wa Mataifa, wakati Yeye amekuja kupitia kwa watengenezaji na kadhalika, hata mwisho, na kuahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Ibrahimu, ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa kwa Mataifa katika siku ya mwisho.” Yeye angerudi tena.

¹²⁹ Mengi sana yangeweza kusemwa hapa, lakini hebu niharakishe sasa kwa sababu ni—ni saa tatu, imepita kidogo tu. Tutatoka ifikapo saa tatu na nusu, Bwana akipenda.

¹³⁰ Angalieni, nabii alisema, huku katika Zakaria 14:6, “Kutakuwako na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, bali itakuwa ni siku yenye utusitusi; lakini katika wakati wa jioni, kutakuwako Nuru.” Sasa angalieni, upesi. Hakuna Maandiko yanayoweza kuvunjwa. Yote hayana budi kutimizwa.

¹³¹ Sasa jua huchomoza vipi? Huchomoza wapi? Mashariki. Linatua wapi? Magharibi. Ustaarabu umesafiri pamoja na jua, na vivyo hivyo na Injili. Mnalipata? Sasa tumerudi kwenye Pwani ya Magharibi sasa tena. Tukisonga mbele zaidi, tunarudi moja kwa moja Mashariki tena, tuvuke Pasifiki moja kwa moja kwenda Mashariki tena; hakuna kitu pale, mnaona. Sasa ustaarabu umesafiri pamoja na jua.

¹³² Injili imevuka bahari. Ilitoka—ilitoka Mediterania, kisha ikavuka ikaingia, kutoka kwa Mtakatifu Paulo hadi Ujerumani, kutoka Ujerumani, ilivuka mlangobahari wa Uingereza, hadi Uingereza; kutoka Uingereza, ikavuka Atlantiki, ikaingia Marekani, na sasa imerudi tena kwenye Pasifiki.

¹³³ Angalieni, jua lile lile linalochomoza Mashariki ndilo jua lile lile linalotua Magharibi, j-u-a. Na Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, kule Mashariki...Sasa imekuwa ni siku ambayo isingaitwa mchana, ni ya utusitusi, siku yenye utusitusi, yenye mvua; mnaiona hapa Kansas, yenye mvua, yenye utusitusi. Tumekuwa na nuru ya kutosha ku—kujiunga na kanisa, na kufanya mambo haya, nuru ya kutosha kutembea huku karibu, bali Yeye alisema, “Wakati wa jioni, itakuwa Nuru, Mwana angerudi tena.” Na Roho Mtakatifu anarudi katika siku hizi za mwisho pamoja na utimilifu tena wa nguvu za Mungu; Neno likidhihirishwa! Kupitia Walutheri...

¹³⁴ Na kama tu ninii—kama tu piramidi inavyokua. Lutheri, matengenezo ya kwanza; Wesley; Pentekoste; na sasa inachongwa ipate kuingia moja kwa moja. Kwa kuwa, wakati Jiwe la Kifuniko litakaporejea kwenye Piramidi, italibidi kuenea kama hayo mengine. Hata huwezi kuupitisha ubapa wa kisu katikati yake, ni kamilifu sana. Na vivyo hivyo huduma katika siku za mwisho, itafanana sana.

¹³⁵ Ni kama vile mkono wa—wako ulivyo ni halisi, na ki—kivuli cha mkono wako kikiwa negativu; vinapokuja, baada ya kitambo kidogo, vinakuwa ni kitu kimoja. Vinakuwa hivyo. Na hivyo ndivyo Kanisa linavyokuwa, Bibi-arusi anavyokuwa kwa Kristo, wanakuwa ni mmoja, kama vile mwanamume yeyote na mkewe. Mnaona? Anakuja moja kwa moja kufikia kwenye siku za mwisho, nasi tunajaribu kuishi katika mng'ao wa siku nyingine? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, inamtambulisha Yeye kikamilifu kabisa na Waebrania 13:8, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹³⁶ Kama tungaliishi huko nyuma katika wakati wa Luther, tuangalie papa hapa nyuma katika—katika wakati huo, tunaona hasa, katika wakati huo wa Sardi, ya kwamba Luther alikuwa ndiye huyo mjumbe, hakika kabisa, pamoja na yule farasi aliyetoka, pamoja na hao wengine waliotoka katika wakati huo.

¹³⁷ Tunaona wakati wa Wesley, ule wakati wa Filadelfia. Tunaona huo wakati mkuu wa uamsho ulioendelea, upendano wa ndugu, tunamwona Wesley akiwa mahali pale pale hasa ambapo Biblia ilisema alikuwa.

¹³⁸ Tunaona siku hizi pale pale tu Yeye alisema alikuwa. Hii ndiyo ile saa, wakati tunamoishi.

¹³⁹ Sikilizeni, wale Wayunani walishindwa kumwona. Kwa nini? “Mabwana, tungetaka kumwona Yesu.” Walishindwa kumwona kwa sababu Yeye alikuwa amevaa hekalu Lake la kibinadamu, Mungu katika mwanadamu, Mwili wa binadamu ndio uliowapofusha. Wasingeweza kufahamu. “Wewe, ukiwa ni mwanadamu, unajifanya Mwenyewe Mungu, ama sawa na Mungu.”

¹⁴⁰ Akasema, “Vema, kama mngeweza kuwaita kwa torati, wala hakuna Maandiko yanayoweza kutenguka, mnawaita ‘miungu,’ walikuwa miungu, ambao walijiliwa na Neno la Mungu.”

¹⁴¹ Basi, Yeye Ndiye utimilifu wa hilo Neno, Neno lililokuwa ni kwa ajili ya siku hiyo, Mwana wa Mungu, Mkombozi; wakati Mungu, Mwenyewe, Yeye alikuja duniani na kuishi katika Mwanadamu, apate kuyachukua mauti juu ya nafsi Yake, apate kuwakomboa wote, ule Mti kutoka kwenye bustani ya Edeni, sio yule mwanamke; yule Mwanamume, Adamu wa pili ambaye alikufa na kuingia ardhini, apate kutoa hizo kemikali, amina, hayo majani yaliyokuwa yameanguka huko nyuma, apate

kuyaleta katika ufufuo. Ni mengi jinsi gani yangesemwa juu ya jambo hilo, ingetuchukua saa nyingi!

¹⁴² Lakini tupo hapa penyewe sasa. Wamataifa wa siku hizo walishindwa kuliona, kwa sababu lilikuwa katika mwili wa kibinadamu. Sijui kama tutafanya jambo lile lile. Sijui kama tutafanya kosa hilo la kuhuzunisha ambalo walilifanya, kushindwa kumjua Yeye? Kwa sababu, Yeye alikuwa, Yeye Neno kwa ajili ya wakati huo, alitambulishwa katika mwili wa mwanadamu. Mvulana ambaye hakuwa na elimu, ambaye hatukumjua akienda shuleni. Hatukuwa na vitambulisho hata alipata kutoka kwenye dhehebu lolote la siku hizo; bila elimu. Hakuwa na sifa za chochote, lakini, “Mwendawazimu, mlevi, rafiki wa wenye dhambi, Mtu anayeupindua ulimwengu; aliyezaliwa kiharamu, mama Yake alitiwa mimba na askari, Naye akajichukulia jina kama Mwana wa Mungu, ama kujiita Mwenyewe nabii, Mgalilaya huyu, anayejiita nabii.”

¹⁴³ Lakini Neno lilidhihirishwa! “Wote waliompokea, Yeye aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu.” Na ndivyo ilivyo siku hizi, wakati tunapoiona kazi hii kuu ya Roho Mtakatifu ikidhihirishwa, “Wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika wana na binti za Mungu.” Yesu Kristo akitambulishwa vile vile, kwa Neno Lake, katika kila kizazi.

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

¹⁴⁴ Marafiki Wakristo, ninataka kuwaulizeni, hebu na tusimame tuwazie kwa muda kidogo. Je! hii ni Kweli ama ni kosa? Ndivyo ilivyo? Kama ni Kweli, tunawajibika kwa yote. Tunaenda wapi? Mwisho wa jambo hili ni wapi? Unawezaje kuwa na hakika ya kwamba unasema kweli? Sasa, “hapo mwanzo, Yeye alikuwa ni Neno,” nalo Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni. Lilifanya hivyo kupitia kwa manabii, lilifanya hivyo kupitia kwa Kristo, Naye aliliahidi katika siku za mwisho, kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁴⁵ Baba wa Mbinguni, lichukue Neno Lako, ukaliweke katika moyo wa mwanadamu, kusudi wao . . . watu wote pamoja, usiku wa leo, kundi hili dogo la watu hapa nje. Tunatambua, Bwana, ya kwamba tunaninii—tunaishi katika vivuli vya Kuja Kwake, navyo vivuli vinakuwa halisi zaidi, mwaka baada ya mwaka. Tunaona ishara zikitokea, mambo ya kutisha. Tunayaona kwenye magazeti ya kila siku na magazeti ya muda. Mwezi unageuka kuwa damu. Tunasikia juu ya matetemeko ya nchi kote ulimwenguni, yakiulipua ulimwengu mzima.

¹⁴⁶ Na, sasa, siku moja yaliutikisa ulimwengu mzima, wakati Mwana wa Mungu alipokataliwa rasmi na kusulibishwa. Na sasa tunaona ya kwamba kundi kubwa, linaloitwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni, limemtoa nje rasmi, kama walivyosema katika ninii (huu) Wakati wa Laodikia, “Alikuwa nje ya kanisa, akibisha mlangoni, akijaribu kurudi ndani.” Na sasa tunaona

ya kwamba kuna tetemeko lingine ambalo liliikumba hii, si mataifa mengine, taifa hili, likautikisa ulimwengu mzima; Yesu akitolewa nje rasmi. Naye anasimama akisihi, usiku wa leo, ametambulishwa kinaganaga, yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁴⁷ Jalia waaminio walione. Jalia wale walio wagonjwa walione, Bwana. Jalia wale walio hapa usiku wa leo waweze kuligusa vazi Lake, kama walivyofanya katika siku zilizopita. Waponye wagonjwa, na uwaokoe waliopotea, tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu awabariki.

¹⁴⁸ Sasa hebu dakika moja kwa ajili ya mstari wa maombi. Tuna dakika kumi na tano kamili, za kutoka katika wakati mzuri. Sasa yote ningaliweza kusema, mimi ni mwanadamu, maneno yangu yanaweza kushindwa kama tu ya mtu yeyote mwingine, sisi sote. Nimewathibitishia usiku wa leo, ya kwamba kila nabii, chochote kile, walifanya makosa yao. Lakini Mungu hafanyi makosa yoyote. Neno Lake ni Kweli. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yeye ni Neno? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu awabariki. Hapo ndipo imani yangu imejengewa, si juu ya kitu chochote pungufu ya Damu ya Yesu; na, kweli, Yesu ni Neno.

¹⁴⁹ Sasa ninaamini ya kwamba Billy alisema . . . Je! alisambaza kadi za maombi? Ku—kuna kadi za maombi zilizotolewa? Sikujua. Yeye—yeye alisema, kwanza, ya kwamba hakudhani walikuja na kusambaza yoyote. Lakini kama walizisambaza kadi za maombi, tutafanyiza mstari mfupi wa maombi.

¹⁵⁰ Mtu fulani, je! hapa kuna kadi ya maombi namba moja? Hebu tuone ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja. Naam, una namba moja? La. Kadi ya maombi namba moja, ni nani aliye nayo? Kuna kadi ya maombi namba moja? Vema, labda hakuzisambaza kutoka namba moja. Ni wangapi. . . En-he? [Mtu fulani anasema, "Hii hapa namba moja."—Mh.] Loo, ipo? Naam. Vema, Kadi ya maombi namba moja, njoo hapa usimame karibu nami hapa, kadi ya maombi namba moja.

¹⁵¹ Namba mbili, ni nani aliye na namba mbili? Namba tatu. Kwa dakika chache sasa, sisi. . . Namba tatu, ni nani aliye na kadi ya maombi namba tatu? Angalieni, kuna mtu hapa kwenye machela, mtu fulani na aangalie kadi yao, kama wana moja. Namba tatu. Namba nne, nne, ni nani aliye na kadi ya maombi namba nne?

¹⁵² Ni kadi ndogo. Mwanangu ama mmoja wa kundi hilo atashuka aje na kuzichukua kadi hizi, mbele zenu, na kuzichanganya zote, kisha wanawasambazia. Ndipo wakati ninaponinii. . . Basi hiyo inaonyesha. . . Tulikuwa na watu wakati mmoja waliojaribu kuziua hizo kadi za maombi, na hiyo ndiyo sababu zinatambulishwa jinsi hiyo, hata huwezi, huwezi kuziua; maana hawezi, hujui ni nani atakayekuja kule. Nijapo

hapa, sianzii kwenye namba fulani maalum. Huanzia tu kutoka mahali popote. Kote katika juma hili, mtaona, nitabadilisha, nyuma kwenda mbele, na juu na chini, kupata kadi hizi za maombi, mnaona. Na kwa hiyo tunafanya jambo hilo hivyo, ili kusema ya kwamba kila mtu kwa kila siku, tunapozisambaza hizi kadi, ili kwamba watu kila siku wanaweza kupata nafasi ya kuingia.

¹⁵³ Moja, mbili, tatu, nne, tano. Nitawaita mmoja mmoja, maana sitaki mtu fulani awe ni kiziwi kisha waseme, “Mbona, hakuna mtu aliyeniambia,” mnaona, nao wakakosa mahali pao kwenye mstari wa maombi. Na labda, wakiwa na kadi ya maombi, wasingewapa nyingine, mnaona.

¹⁵⁴ Kadi ya maombi namba tano, ni nani aliye nayo? Moja, mbili, tatu, nne, tano. Kadi ya maombi tano? Hiyo ni sawa. Kama una hakika una tano, nenda pale juu. Hiyo ni sawa. Namba sita? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kumi na moja, kadi ya maombi kumi na moja. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kadi ya maombi kumi, na kumi na moja.

¹⁵⁵ Angalieni sasa, huenda ikawa ni mtu aliye kiziwi. Angalia kadi ya jirani yako. Kila mahali. Nafikiri zote zimechanganywa kote kupitia hapa. Vema. Ni wangapi waliopo hapo, Roy? Wahesabu uone. Kumi na moja? Kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Moja, mbili, tatu, nne. . . Kumi na watano. Vema. Hebu na tuachie papo hapo kwa dakika moja tu, maana hatuna muda mwingi sana.

¹⁵⁶ Sasa ni wangapi wasio na kadi ya maombi nawe unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, inua mkono wako. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli, kuwa na imani hiyo. Sasa kumbukeni, marafiki, wakati wakijiandaa kwa ajili ya mstari wa maombi, sasa, m—m—msisogeesogee sasa, kwa dakika kumi tu ama kumi na tano zifuatazo, mpaka tutakapokuwa tayari, maana, unaona, wewe ni roho.

¹⁵⁷ Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Nilisema, na nikasoma kutoka kwenye Maandiko, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na kwa kipindi kifupi tu, kwanza sijalifanya hilo bado, kuwaonyesha ya kwamba Yeye anapaswa kuchukua jambo lili hili tena katika siku za mwisho. Ni wangapi wanaoamini hilo? Malaki 4 na yote hayo yanapaswa kurudi moja kwa moja tena, Yeye tena kushuka na kujitambulisha Mwenyewe katika Ujumbe wa kinabii, kugeuza mioyo ya watoto irudi kwenye ile Imani; Imani ya mitume, ya pentekoste, ya wale baba zetu. Hilo ndilo hasa linalopaswa kufanywa. Sio kanuni fulani ya imani; bali kurudi kwenye Imani ya kwanza. Sasa tunaamini hilo kwa moyo wetu wote.

¹⁵⁸ Sasa baadhi yenu hapo wasio na kadi ya maombi. Sasa, kumbukeni, mimi ni mtumishi Wake na wewe ni mtumishi Wake,

Mungu ndani yangu na Mungu ndani yako. Una haja, nami nipo hapa kukutumikia, inaleta hayo pamoja na kuyafanya Mungu.

¹⁵⁹ Sasa, maskini mwanamke yule, wakati mmoja. Hebu niwape Andiko jingine, ninaamini kwamba liko katika Yohana Mtakatifu, pia. Kulikuwako na maskini mwanamke mmoja ambaye, alikuwa, alikuwa na ugonjwa wa kutokwa na damu. Hebu tuseme hakuwa na kadi ya maombi, naye alitaka kuombewa. Lakini kulikuwako na wengi sana waliosimama pale, asingeweza kuingia mstarini. Kwa hiyo akasema, “Nikiweza tu kugusa vazi Lake, nitapona.” Ni wangapi wanaoikumbuka hadithi hiyo? Mbona, hakika. Naye alifanya nini? Alisukuma akapitia kwenye umati huo na kugusa vazi Lake.

¹⁶⁰ Sasa, vazi la Kipalestina huning’inia na kupwaya, na lina vazi la ndani, pia, maana mavumbi kwenye miguu, mwajua, kwa hiyo ni ninii. . . linapwaya. Sasa unaweza ukagusa koti la mtu fulani, wala asingehisi kitu, kwenye ncha tu ya koti lake. Lakini vipi kuhusu vazi hilo kubwa, nene, zito la Kipalestina, linaning’inia chini kwenye miguu yake, unaona? Kamwe Yeye hakuhihi huo, kimwili.

¹⁶¹ Lakini aliligusa vazi Lake kisha akarudi kwenye umati huo. Hebu tuseme aliketi chini. Huenda alisimama, bali tuseme aliketi chini. Ni kitu gani kilichotukia? Yesu alisimama na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

¹⁶² Na, unajua, Mtume Petro aliwazia ya kwamba hilo lilikuwa ni la mzaha sana, mpaka watu. . . Mbona, yeye alimkemea kwa sababu ya jambo hilo. Kwa maneno mengine, huenda alisema, “Mbona, angalia, kila mtu anakugusa. Watafikiri hili, ‘Umeharibikiwa na akili.’ Unaona? Mbona, kila mtu anajaribu kukugusa, Rabi.”

¹⁶³ Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa mnyonge. Nguvu,” yaani uweza, “umenitoka.”

¹⁶⁴ Maskini mwanamke huyo mmoja alichomoa nguvu kutoka Kwake. Aliangalia kila mahali katika wasikilizaji hao na kupata mahali alipokuwa, na akamwambia shida yake na kile kilichokuwa kimetukia. Biblia ilisema kwamba, “Yeye sasa ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.” Hiyo ni kweli? Sasa kama wewe una imani ile ile katika Yesu yuyo huyo, itakufanyia jambo lile lile.

¹⁶⁵ Sasa iweni wenye kicho kwelikweli. Ombeni. Msitilie shaka. Aminini kwa moyo wenu wote ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye atawajalia baraka hizi.

¹⁶⁶ Sasa, Baba, jalia Roho Wako Mtakatifu mkuu atufunulie Neno lililotambulishwa katika mwili, miili yao na mwili wangu. Na jalia Neno na ahadi ya Injili ya usiku wa leo, ambalo limehubiriwa, lifasiriwe na Roho Mtakatifu Mwenyewe aliye mkuu, kwa kuwa Yeye aliahidi angekuwa pamoja nasi. Naye ni

yeye yule jana, leo, na hata milele. Katika Jina la Yesu Kristo, tunajikabidhi Kwako, pamoja na Ujumbe, upate kulithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata, kama ulivyofanya kulingana na Marko 16. Amina.

¹⁶⁷ Sasa kila mtu na awe na kicho sana. Naomba msisogee. Ketini kimya kabisa, mnaona. Sasa, kumbukeni, wakati mwingine tumefikia mzozo. Ni wangapi walio humu ndani ambao ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili, hebu tuione mikono yenu. Vema, hilo ni sawa, basi mnajua ninalozungumzia.

¹⁶⁸ Sasa, je! huyu, ndiye mama huyo? Huyu ndiye mama wa kwanza mstarini. Vema. Sasa, mimi na mama huyu, nijuavyo mimi, hatufahamiani, picha nzuri sana ya Yohana Mtakatifu, mlango wa 4. Yesu alikutana na mwanamke kwenye kisima cha Samaria, mandhari kama haya, mara ya kwanza waliyopata kukutana maishani. Na kadiri nijuavyo mimi, hii ndiyo mara ya kwanza tumekutana. Sisi hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, kusudi tu watu waone kwamba hiyo ni kweli, inua tu mkono wako. Kwa hiyo mnaona, sisi hawa, mara ya kwanza.

¹⁶⁹ Sasa kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, sasa kuzungumza na mwanamke huyu, jinsi alivyofanya na yule mwanamke pale kisimani, ingekuwa ni kutafuta kujua jambo fulani ambalo amefanya, ama shida yake, ama kitu juu ya ninii. . . kitu ambacho sijui lolote kukihusu, naye angemfunulia. Ambapo, sijapata kumwona, mimi ninaninii tu. . . mara ya kwanza niliyopata kuwa humu jijini. Nami nipo tu hapa, yeye ni mgeni. Sasa hilo lingemfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele? Hilo lingelifanya Neno kuwa lenye kutambua mawazo yaliyo moyoni? Mnaona? Mnaona? Lingemfanya yeye yule jana. . .

¹⁷⁰ Basi hii hapa mikono yangu, na Biblia yangu, sijapata kumwona mwanamke huyu maishani mwangu. Mungu anajua hilo. Yeye ni mwanamke tu anayesimama hapo. Si—sijui zaidi juu yake kuliko mtu aliye mgeni kuliko wote aliye hapa ndani, kwake. Hiyo ni kweli, naye anajua hilo.

¹⁷¹ Simjui; ila Yeye anamjua. Naye ni Neno, nalo Neno huifunua siri ya moyoni, linasema mambo, mabaya, linamwambia kitu. Kama amefanya lolote baya, halijatubiwa chini ya Damu, Yeye atamwambia kuhusu hilo. Kama yeye anajifanya mwaminio, Yeye atamwambia kuhusu hilo. Kama yeye ni mwaminio, Yeye atamwambia kuhusu hilo. Kama kuna shida yoyote ya mwili, Yeye atamwambia kuhusu hiyo. Kama yeye ni kitu fulani kwa ajili ya kitu kingine, atamwambia kuhusu hicho. Anaweza kufanya yote hayo, maana Yeye ni Mungu. Anajua mambo yote. Sijui mimi; yeye hanifahamu wala mimi simfahamu. Sasa kama Yeye akilifunua hilo kwa njia hiyo, mnajua lingali ni Neno, Waebrania 4:12, “Neno la Mungu huzifunua siri za moyoni, na linajua hali za mambo.”

172 Sasa kama Mungu ataninii—atatufunulia jambo hili usiku wa leo, dada, wakati mimi na wewe tumesimama hapa pamoja, basi ungeninii—ungejua isingeweza kuwa ni mimi. Ingebidi iwe ni Yeye. Sasa ninataka kuzungumza na wewe tu kwa dakika moja, kwa sababu kuzungumza katika Neno namna hii. Mbona, mimi ninahubiri, unaona, na halafu ninarudi, ninazungumza tu na wewe kama Yeye alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, akazungumza naye mpaka akapata kujua shida yake ilikuwa ni nini. Sasa kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, vema, utajua kama ni kweli ama si kweli.

173 Na hivi nyote mtaamini? Kuna mtu yeyote huko nje anayemjua mwanamke huyu? Inua mkono wako kama wapo watu wowote...Loo, naam, watu wengi sana wanamjua. Naam. Vema.

174 Sasa Bwana Yesu na ajalie jambo hili, mnaona. Hilo lisingekuwa tu ni Neno lililohubiriwa, lingeekuwa ni Neno lililofanyika mwili, likinena, likifunua. Sasa Biblia haisemi ya kwamba utakuwa umesimama hapa, na kwamba utakuwa una shida gani, na yote kulihusu, na kilichokuleta hapa, ama yale umefanya. Haisemi hilo. Lakini Neno hushuka, linalomtambulisha msemaji, mnaona, ya kwamba Neno la Mungu; basi Ujumbe ni wa kweli, basi Mungu anautambulisha Ujumbe kwamba ni wa Kweli. Ubatizo wa Roho Mtakatifu na Injili yote hazina budi kuwa ni Kweli basi, kama likitambulishwa vizuri.

175 Jambo moja, wewe una wasiwasi mwingi sana, wasiwasi kweli. Umefadhaishwa na jambo fulani. Hiyo ni kweli. Una wasiwasi. Umeekuwa nao kwa kitambo fulani. Na jambo ni kwamba, ni ugonjwa wa mguu wako. Liko kwenye mguu wako wa kulia. Unahofu ni kansa. Inakusumbua kila mahali. Upande huo wa kulia umekwisha kabisa. Unasumbuliwa na tumbo lako, linakuchefua. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Usiogope, amini tu Naye atakuponya. Unaamini hayo? [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, nenda ukimshukuru Mungu kwa ajili ya hilo, na uwe mzima. Bwana akubariki. Ninataka tu kukuwekea mikono.

176 Je! mnaamini ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

177 Sasa hii hapa picha tena, mzungu, mwanamke mweusi. Yesu akiwa ni Myahudi, yeye Msamaria; mnaona, Yeye aliwafanya wajue hakuna tofauti katika jamii ya wanadamu. Mungu alitufia sisi sote. Hiyo ni kweli. Yeye ni . . . “Mungu aliyafanya kwa damu moja, mataifa yote.” Nchi tulimolelewa, iliibadilisha rangi yetu, haikuwa na uhusiano wowote na kile kilicho ndani yetu. Naam, hiyo ni kweli.

178 Sasa wewe ni Mkristo. Upesi ninaweza kuhisi ile hisi ya kule kukaribishwa, kwamba wewe ni Mkristo. Hiyo ni roho yako.

Hiyo ingekuwa tu ni kama Yeye alivyosema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, hamna hila ndani yake.”

¹⁷⁹ Sasa, ninaona umekuwa mgonjwa sana. Uchunguzi unathibitisha ya kwamba una kansa. Hiyo ni kweli. Na kansa hiyo, je! unaamini anaweza kuniambia mahali ilipo? Kulingana na takwimu, kansa hiyo imo katika utumbo mpana. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa unajua ya kwamba Kitu fulani kimesimama hapa ambacho kinakujua. Unaamini ya kwamba atakuponya? Kama imani yako inaweza kumvuta huko, kuligusa vazi Lake na kufunua jambo lile lile alilofanya wakati ule, basi nenda ukamwamini nawe utapona kutokana na huo, na kupata afya. Kama utaamini jambo hilo, amini tu, ni rahisi tu hivyo, dada, kuamini tu. Usitilie shaka.

¹⁸⁰ Nafikiri sisi hatufahamiani, pia, mimi na wewe? Hatufahamiani. Mungu anatumjua sisi sote. Unaamini ya kwamba Mungu angeweza kunifunulia shida yako? Unaamini angeweza kunifunulia shida ya mtu yeyote huko nje? Unaamini jambo hilo?

¹⁸¹ Ni wangapi huko nje wanaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁸² Unawazia nini juu ya jambo hilo? Unaamini kwa moyo wako wote? Basi mawe yako ya nyongo hayatakusumbua tena. Ni—nililisikia likija, nilikuwa “nikisoma mawazo ya watu,” nilitaka tu mwone sikuwa nikiyasoma.

¹⁸³ Vema, unaniamini mimi kwamba ni mtumishi Wake? [Dada anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Kwa moyo wako wote? [“Kwa moyo wangu wote.”] Asante. Wewe ni Mkristo. [“Ndivyo.”] Naam, ndivyo, wala si mwomba lifti; Mkristo halisi, na umezaliwa mara ya pili. Vema. Je! unaamini ya kwamba—ya kwamba mimi, nikiwa ni ndugu yako, sijui lolote kukuhusu; lakini Baba yetu wa Mbinguni, anayetujua sisi wawili, angeweza kunifunulia shida yako ni nini? [“Ninaamini.”]

¹⁸⁴ Ninaona ya kwamba umekuwa na nyingi sana. Umefanyiwa upasuaji, na huo upasuaji ulikuwa ni wa kansa. Ulitoa ziwa, hiyo ni kweli, na ungali unasumbuliwa nayo. Unaamini utakuwa mzima tangu sasa na kuendelea? Pitia papa hapa, ukiamini kwa moyo wako wote. Na Mungu akubariki, Bwana Mungu na akuponye. Hebu. . .

¹⁸⁵ Kuwa na imani. Usitilie shaka. Amini tu kwa moyo wako wote ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸⁶ Sasa je! unaamini, mama? Hatufahamiani. Sikujui. Hunijui mimi. Hatufahamiani kabisa. Lakini Baba wa Mbinguni angenifunulia jambo fulani baya, jambo ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya, ama ulilopaswa kufanya wala hukulifanya, lolote lile, lolote liwalo, utaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unajua ingepaswa kuwa ni Yeye ambaye angefanya hilo. Hiyo ni kweli?

¹⁸⁷ Unasumbuliwa na ki—ki—kivimbe, na kivimbe hicho kiko kichwani. Una hofu sana. Kweli. Unaamini ya kwamba kitatoka sasa, ya kwamba Yesu Kristo atakupa afya? Kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako. Nenda ukiamini. Amina. Mungu akubariki. Nenda zako tu, amini. Kamwe, usitie shaka. Amini tu kwa moyo wako wote.

Kuwa na imani. Usitilie shaka. Amini tu kwa moyo wako wote.

¹⁸⁸ Tumbo lako limekuwa likikusumbua. Ugonjwa wa tumbo. Unataka kwenda kula? Amini. Haya basi.

¹⁸⁹ U hali gani? Hatufahamiani. Sikujui, hunijui. Lakini pana mtu fulani hapa, asiyeonekana, lakini ametiwa utaji katikati yetu, anayejua shida yako ni nini. Ninakuona ukijaribu... Naam, ni yabisi kavu. Unaamini atakuponya kutokana na hiyo? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nenda, amini hilo, wala hautakulemaza kama utaamini tu.

¹⁹⁰ Una mambo mengi ambayo yamekusumbua. Shida ya akina mama, kwa muda mrefu; halafu, jambo lingine, kitu cha—chako kikuu ambacho unataka kuponywa, ni yabisi kavu, pia. Unaamini ya kwamba atakuponya? Nenda zako, amini. Hakuna lingine, kuwa tu na imani na usitilie shaka.

¹⁹¹ Hunifahamu mimi. Sijapata kukuona maishani mwangu. Kuna mwanamke mwingine ambaye anatokeatokea. Kama Mungu atanifunulia jambo fulani kukuhusu wewe... Naam, naam, ni uvimbe; anakabiliwa na upasuaji. Maskini mwanamke yule aliye kwenye kile kiti anakabiliwa na jambo lilo hilo, ni kivimbe. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini? Mungu atawaponya ninyi nyote wawili kama mtaamini jambo hilo. Weka mkono wako juu yake. Jambo ndilo hilo. Katika Jina la Bwana Yesu, katika Jina la Bwana Yesu, na uponywe, dada.

¹⁹² Mnaona, ninyi, siwezi kulielezea hilo, marafiki, msiniulize kulieleza. Presha, nguvu, mmoja... Kivimbe ni kitu gani? Ni kikulia. Kikulia ni kitu gani? Kuzidishwa kwa seli. Wewe ni nini? Kuzidishwa kwa seli. Kivimbe ni kitu gani? Katika Biblia, kinaitwa ibilisi, mtesi; hebu mwone akiomba msaada kwa kupiga makelele, naye huyo mwingine akamjibu. Mnaona, wawili waliofanana, na hilo ni—hilo ndilo lililolisababisha. Vema.

¹⁹³ Njoo, mama. Hatufahamiani. Umekuwa na hali ya wasiwasi kwa muda mrefu sana, ambayo imekufanya kushikwa na ugonjwa wa tumbo, shida ya tumbo, kidonda cha tumbo, kulichachua tumbo lako, na kuathiri meno, na kadhalika. Unaamini kwamba Yesu Kristo atakuponya sasa? [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, nenda ukale chakula chako cha jioni basi. Amini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakufanya mzima. Amini tu sasa. [“Haleluya! Asante, Yesu.”]

194 Hatufahamiani. Mungu anaishi wapi katika mwanadamu? Moyoni. Hapo ndipo ilipo shida yako, iko kwenye moyo wako, si kwa sababu ya kumkosa Mungu. Bali ni kuachilia imani yako, kuponya ugonjwa huo wa moyo, nawe utapona. Nenda zako, ukiamini, amini kwa moyo wako wote. Sasa, usitilie shaka. Nenda, ukiamini.

195 “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Ni wangapi wanaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaamini ya kwamba Mungu yupo hapa kukufanya mzima? Unaninii... Je! Neno limefanyika mwili? [“Amina.”] Ni kitu gani? Sasa, haidhuru ninaamini kiasi gani, wewe huna budi kuamini, pia. Mnaona, yule mwanamke aliyegusa vazi lake, aliamini.

196 Huyu hapa mwanamume anayeketi hapa akiniangalia. Ana ngiri na bawasiri. Unaamini Mungu atakuponya? Kama unaamini, unaweza kupata ulichoomba.

197 Mtu mwingine hapa ndani anayeamini ya kwamba Mungu huwaponya wagonjwa na wanaoteseka? Unaamini ya kwamba Neno, usiku wa leo, linajua siri za moyo? Unaamini jambo hilo? Vema. Ni kwamba sasa tumechelewa sana kwa yale tuliyokuwa.

198 Ungeaminije jambo hili? Sasa unajua ya kwamba Maandiko yanafanywa dhahiri, usiache pazia la mwili likusumbue sasa, unaona. Kumbuka, ni Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hizi. Ni wangapi wanaofahamu hilo? Neno lililoahidiwa. Sijui mmeona maigizo kiasi gani. Lakini, naomba heri, Yesu Kristo aliahidi jambo hili, na hili ni kweli. Mnaona, hilo, hilo ni kweli.

199 Sasa je! Yeye husema pia, yale maneno ya mwisho aliyosema kabla hajaondoka duniani, akapaa Mbinguni, alisema, “Enendeni ulimwenguni kote,” Marko 16, “mkaihubiri Injili. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio”? Ulipata kusoma hayo? Agizo la mwisho lilikuwa ni nini? “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ni wangapi wanaojua jambo hilo kwamba ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.—Mh.]

200 Sasa kila mmoja wenu, dakika chache zilizopita, uliinua mkono wako kwamba ulikuwa ni mwaminio. Sasa si mwekeane tu mikono hapo? Haitatubidi kuendelea; mnajua Yeye yupo hapa, mbona msiwekeane tu mikono ninyi kwa ninyi na kumwombea mtu huyo anayeketi karibu nawe, kama wewe ni mwaminio. Sasa, Yeye alisema! Sasa, la, si mimi peke yangu; ni wewe, kila mmoja wenu. Mnaliamini sasa? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

201 Sasa, angalia, usijiombe wewe mwenyewe, kwa maana mtu aliyekuwekea mikono anakuombea. Unaona, wewe waombe, nami nitawaombea ninyi nyote. Na kama tu mtaamini, kwa

moyo mmoja, huu utakuwa ni mmoja wa nyakati kuu sana mlizopata kuona.

²⁰² Uwepo wa Yesu Kristo, ambao unapaswa kuliangaza kanisa, kujua ya kwamba katika siku hizi za mwisho ambapo kanuni za imani na madhehebu, na itikadi na kila kitu zimelisonga Ne—Neno kabisa, na Yesu aliye Neno yuko nje ya kanisa, nanyi mnamwona akirudi moja kwa moja miongoni mwa watu na kujitambulisha Mwenyewe kama alivyoahidi, “katika siku za mwisho wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.” Yeye alifunuliwa katika ubatizo; alifunuliwa katika uponyaji wa Kiungu; Huyu hapa katika sifa Yake ya mwisho. Kumbukeni, hilo lilikuwa ndilo jambo la mwisho ambalo Ibrahimu aliona kabla ya moto kushuka na kuuhukumu ulimwengu wa Mataifa, na kabla yule mwana wa ahadi hajajitokeza jukwaani, Isaka. Hili ndilo jambo la mwisho ambalo kanisa la Kikristo litaliona, katika ishara ya muujiza, mpaka kule kuonekana kwa Yesu Kristo. Kama Mungu amenipa kibali mbele yenu, niaminini katika Jina la Bwana, hakuna kitu kingine kilichosalia katika Biblia kutendeka ila kuichukua alama ya mnyama; ninyi mna Muhuri wa Mungu.

²⁰³ Mwombee mtu huyo aliyelala hapo, anayeketi karibu nawe. Wawekee mkono wako. Ni—nilikuwa nikiwatafuta vilema; sioni wowote. Lakini kitanda hicho kidogo, ninaamini, tayari kimeninii, loo . . . Vema, wekeaneni mikono na mwombe.

²⁰⁴ Mpenzi Yesu, Mwana mkuu asiye na dhambi wa Mungu aliye hai, ambaye yupo hapa usiku wa leo katika umbo la Roho Mtakatifu, alibadilisha umbo Lake na akashuka chini na kulifunua Neno Lake moja kwa moja katika mwili wa binadamu; mwanamume, wanawake, wa kila tabaka la maisha, akionyesha ya kwamba angali hai. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

²⁰⁵ Bwana Yesu, tupo hapa katika jiji hili kuu la Topeka, tupo hapa tumekusanyika pamoja na watoto Wako. Nasi tunaomba, ya kwamba kwa kuwa umejitambulisha sana miongoni mwetu, kwamba sasa utalithibitisha Neno Lako, lile agizo la mwisho, ukisema, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapona.” Nao watu, wenye kukiri, na kuzaliwa mara ya pili na Roho, sasa wanawekeana mikono, kujitambulisha mmoja kwa mwingine, pamoja na agizo Lako na Neno Lako.

²⁰⁶ Sasa, Shetani, huwezi kuwashikilia hawa watu wagonjwa zaidi. Hao ni raia wa Neno la Mungu. Ondoka kwao, ugonjwa ulio mwilini mwao. Usiwatese tena. Waachilie, tangu usiku wa leo na kuendelea. Sisi, kama watumishi wa Mungu, ambao wametambulishwa kulithibitisha Neno, tunakuagiza katika Jina la Mungu aliye hai, Yesu Kristo aliye Neno lililofanyika mwili miongoni mwetu, watoke watu hawa wagonjwa, na uwaache waende, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, na amri tuliyoopewa na Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Amina.

²⁰⁷ Nyote mnaoamini na mnaukubali uponyaji Wenu, bila tashwishi yoyote, hapa ndani ya pazia la Utukufu wa Shekina, kuona Neno lililoahidiwa ambalo tutaliingilia kindani zaidi juma hili, tulione likidhihirishwa papa hapa mbele yetu, hebu tusimame kwa miguu yetu na kusema, “Ninakubali uponyaji wangu sasa. Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo sasa aniponya. Kwa moyo wangu wote, ninaliamini. Ninalikubali, katika Jina la Yesu Kristo.” Mungu awabariki. Inueni mikono yenu sasa. Na kila mmoja wenu, katika njia yako mwenyewe, mpe shukrani kwa ajili ya uponyaji wako. Amina.



KRISTO ALIYETAMBULISHWA KATIKA NYAKATI ZOTE SWA64-0617

(The Identified Christ Of All Ages)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 17 Juni, 1964, katika Ukumbi wa Manispaa huko Topeka, Kansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org